

## Office of Fair Trading

# Kutoa masoko ya haki na salama kwa wakazi wa Queensland.

Tunatoa maelezo muhimu na ushauri kuhusu haki na majukumu yako kama mtumiaji au biashara inayoendesha katika Queensland.

### Wasiliana nasi

Kwa huduma za ukalimani, piga simu kwa 1800 512 451. Tunaweza kutoa huduma za ukalimani za simu bila malipo au uso kwa uso ili kukusaidia kufikia maelezo na huduma za Biashara ya Haki.

Tovuti yetu ina maelezo mengii kuhusu haki na majukumu yako kama mtumiaji au biashara katika Queensland. Tembelea tovuti yetu kwenye [www.qld.gov.au/fairtrading](http://www.qld.gov.au/fairtrading).

### Kununua bidhaa na huduma

Weka vidokezo vifuatavyo akilini wakati unaponunua:

- Unda bajeti na utumie vizuri. Usinunue kwa msukumo na ujaribu kuokoa fedha zako kwa ununuzi mkubwa ujao.
- Fanya uchunguzi na utafiti kabla ya kununua.
- Fahamu haki na majukumu yako ya fidia.
- Soma na hifadhi kazi yako kwenye karatasi. Hakikisha umesoma sheria na masharti yote kabla ya kutia saini mkataba wowote.
- Ikiwa una tatizo na bidhaa au huduma ulizonunua, wasiliana na biashara hiyo ili kujaribu kuitatua. Kama bado hujafanikiwa, wasiliana nasi kwa msaada wa kutatua mzozo.

### Una haki ya kisheria ya fidia, kubadilishwa au ukarabati wa bidhaa au huduma kama bidhaa au huduma:

- haidumu kwa muda unaofaa
- ina dosari ambayo hukujua kuhusu wakati wa ununuzi
- haikufanya kazi ambayo uliamini itafanya
- haiko kama ilivyofafanuliwa na muuzaji au nyenzo ya ukuzaji
- haifanani na sampuli.

Biashara haistahili kukupa fidia kama ukibadilisha nia yako tu, ukichagua kipimo kisichofaa au upate kifaa kingine mahali pengine chenye bei rahisi zaidi.

## **Utapeli**

Kuwa mwangalifu ili uepuke utapeli. Tembelea tovuti ya [www.scamwatch.gov.au](http://www.scamwatch.gov.au) kwa maelezo kuhusu utapeli wa kawaida na jinsi ya kuhakikisha hujapatikana. Kumbuka, kama toleo litaonekana nzuri sana kuwa kweli, pengine ni utapeli.

## **Wachuuzi wa mlango kwa mlango**

Una haki ya ziada wakati watu wa kuuza au wachuuzi wanapokuja nyumbani kwako bila kutarajiwa. Ikiwa mkataba una dhamana ya zaidi ya \$100, una haki ya siku 10 za kutulia, wakati ambao mtu anayeuzza hawezi kuchukua pesa kutoka kwako (pamoja na amana), kuanza kufanya kazi, au kutoa bidhaa na huduma. Unaweza ukakatisha mkataba, kwa kuandika, wakati wowote katika kipindi hiki.

## **Ununuzi wa bei ghali**

Unaponunua vitu vikubwa, kama vile nyumba mpya au gari, tunapendekeza kuwa mwangalifu zaidi. Tovuti yetu ina mwongozo wa hatua kwa hatua wa kununua nyumba. Kabla ya kununua gari lililotumiwa, pata ukaguzi wa PPSR ili kuhakikisha hakuna pesa zilizosalia ambazo mmiliki wa zamani bado anazo.

## **Fedha na mkopo**

Tunaweza kukupa maelezo na ushauri juu ya kununua bidhaa kwa mkopo na kutumia mkopo vizuri. Tunaweza pia kukuelekeza kwa huduma ya ushauri wa kifedha kama una matatizo ya kifedha.

## **Biashara zenye leseni**

Ili kuwasaidia kulinda watumiaji, tunawahitaji wafanya biashara katika tasnia na taaluma hizi kuwa na leseni:

- mawakala wa mali isiyohamishika
- watoa huduma ya usalama
- wachuuzi wa motokaa
- wauzaji mitumba na madalali rahani
- wakusanyaji ushuru na wahudumu wa mchakato
- studio za michoro ya mwili na wasanii
- wahudumu wa utalii
- mawakala wa utangulizi.

Kabla ya kufanya biashara na yejote kati ya wafanya biashara hawa, omba uone leseni zao. Kama hawawezi kuthibitisha kuwa wana leseni halali, usifanya biashara nao. Unaweza kutembelea tovuti yetu ili kufanya ukaguzi bila malipo wa leseni zao.

## **Mashirika yasiyo ya faida**

Ikiwa unahusika katika kuendesha shirika lisilo la faida, unaweza kulijumuisha ili kuwapa wanachama ulinzi wa ziada wa kisheria. Kama utachanga fedha kwa madhumuni ya ufadhilli, lazima ujisajili na sisi.

## **Bidhaa salama**

Tunatoa maelezo mengi juu ya marufuku ya bidhaa zisizo salama, bidhaa zinazostahili kurudishwa ili kurekebishwa na jinsi unavyoweza kuwaweka watoto wako na familia salama wakati unatumia bidhaa zingine. Biashara zote zina jukumu la kuhakikisha bidhaa wanazouza ni salama.